

WAKORINTHO, KITABU

CHA MASAHIHISHO



Habari za asubuhi, marafiki! Nilimwambia Ndugu Neville, nilikuwa kidogo nimepwelewa na sauti asubuhi ya leo, na uamsho huu ujao. Nisingejaribu kuwahubiria asubuhi ya leo, kwa sababu nimepwelewa sana na sauti. Lakini ni kikundi chetu kidogo hapa, huenda nikawa na somo dogo la shule ya Jumapili, kisha nimwache ahubiri kidogo tu. Kwa hiyo tutaninii... Nitakuwa na somo dogo tu kutoka katika Biblia hapa, la jambo ambalo tunaweza kuzungumzia labda kwa dakika kumi na tano, ishirini. Na labda Bwana atatupa kitu fulani kutoka kwa hilo. Sasa, Yeye amekuwa mwema sana kwetu, mzuri sana.

² Na, kwa hiyo, tumechoka. Jana usiku nilichelewa kidogo kulala. Mimi... baada ya mimi... Simu nyingi zikiingia tangu nilipoingia. Ndi—ndipo ilitokea niliona, naye maskini mvulana wangu alikuwa na konzi ya shanga za kioo, akizitafuna tu na kuzila, za kioo, na—na kuzimeza hizi, zilikuwa ni kioo. Na kwa hivyo tukamchukua na kuosha sana maskini kinywa chake. Kisha tulikuwa macho pamoja naye, sehemu kubwa zaidi ya usiku, kwa hiyo kidogo nimechoka asubuhi ya leo.

³ Nami sina budi, saa sita kamili, kuondoka kwenda Kentucky, na kushuka kwenda Kentucky kwenye miadi fulani huko. Na, kisha, juma hili lijalo unakuja mkutano wetu.

⁴ Na sasa nataka kujaribu, siku chache tu usiku za kuzungumza, kama nikiweza. Jamani... Sina mafua hata. Nimehubiri tu sana mpaka sauti yangu imekwisha. Mnaona, hii ni miezi minne, mfululizo, mnaona. Na kwa hiyo basi, baada ya hayo, ndipo ninaenda Canada, na kisha kurudi kwenye mikutano yetu ya kawaida na ya nchi za ng'ambo.

⁵ Sasa, nilipokuwa nimeketi pale, nikizungumza na Leo na Gene, dakika chache tu zilizopita, nilikuwa nikiwazia juu ya Maandiko hapa ambayo huenda tukayatumia asubuhi ya leo. Ikiwa... Sasa, kwanza, nilikuwa nikitaka kuketi pale kidogo, nilikuwa nimechoka sana, ndipo nikawazia, "Hilo halikuonekana sawa, mimi nikiwa nimeketi kule chumbani, na kusanyiko hapa nje. Mbona, Bwana huenda asirudi hapo. Ninataka kuja hapa mahali Yeye alipokuwa."

⁶ Kwa hiyo, naamini ninaona mojawapo ya sababu zilizonileta hapa asubuhi ya leo, Ndugu Littlefield yuko hapa. Naam. Alitaka kuniona muda kidogo tu baada ya ibada. Naye Ndugu Littlefield anatoka Tennessee, kule ambako tulikuwa na ule ninii mkubwa— mkutano mkubwa kule juu, hivi

majuzi kwenye jumba la mazoezi la shule ya upili. Siwezi kukumbuka jina la huo mji. Wapi, wewe, Ndugu Littlefield? [Ndugu Littlefield anasema, “Cleveland.”—Mh.] Cleveland. [“Tennessee.”] Cleveland, Tennessee.

⁷ Na kwa hiyo tulikuwa na wakati mzuri sana kule juu. Naye yuko . . . alikuwa akipitia, kusema “aloo” kwangu, na kwa hiyo nikamwambia ashuke aje asubuhi ya leo. Tulikuwa tunaenda mahali fulani asubuhi ya leo, kwingine, na ndipo, marafiki fulani niliotaka kuwatembelea, si kuhubiri, kutembea tu, maana niliwaahidi. Na ndipo Ndugu Littlefield alikuwa hapa, na Daktari Beeland na hao wengine. Na kwa hiyo nilitaka tu kupitia hapa na kuwaona asubuhi ya leo, ndio sababu ya mimi kuingia.

⁸ Kwa hiyo, sasa, katika Kitabu cha Wakorintho, yapata tu mlango wa 10, na vifungu vya kwanza vinne ama vitano. Hebu tutafakari tu juu ya hivyo kwa muda mfupi, ili ndugu yetu apate wakati wa kuhubiri.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kwanza, katika Uwepo Wake tu.

⁹ Baba wa Mbinguni aliyebarikiwa, kwa kweli ni kwa mioyo ya shukrani ambayo tunainama mbele Zako kwa unyenyekevu leo hii, kukushukuru kwa ajili ya mambo mema ya maisha. Na kutambua kwamba maisha yenyewe ni pambano moja kubwa tu. Ikiwa hatulipati kwa njia moja, tunalipata kwa nyingine, lakini siku moja tukufu vita vitakwisha. Nasi tutamwona Yesu ambaye tumetazamia kumwona tangu tulipompenda, na kufahamiana Naye, na kuwa wa jamaa Yake. Nasi tunafurahi sana kujua ya kwamba siku moja tutamwona.

¹⁰ Sasa, leo hii, tulipoingia chini ya mwaloni wa kale, tuseme, tupate faraja. Kama vile Ibrahimu alivyoketi pale, akingojea, naye Mungu na Malaika wawili wakaja na kuzungumza naye. Nasi tunakutarajia tu uje kwetu asubuhi ya leo, na kunena na mioyo yetu, kupitia Neno Lako, Bwana, tunaposhirikiana Kwalo.

¹¹ Mbariki mchungaji wetu mpendwa, Bwana. Tunaomba kwamba utampa nguvu na ujasiri. Tunaomba ya kwamba utalibariki hili kanisa dogo, na mashemasi na wote wanaohusika hapa, Bwana, na wote wanaokuja hapa; si hapa tu, bali mahali pengine, Kanisa Lako, la ulimwenguni kote.

¹² Wabariki ndugu zetu waliotutembelea walio pamoja nasi asubuhi ya leo katika ibada. Tunaomba kwamba utakuwa pamoja nao na kuwadumisha. Utusamehe dhambi zetu, na useme nasi kupitia Neno Lako. Tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

¹³ Kama sijakosea Ndugu Coats ameketi hapa asubuhi ya leo. Alikuwa . . . kule kumwomba, hivi majuzi usiku, kwenye Hospitali ya Askari Wastaafu; kansa. Nasi tunafurahi kuwaona hapa ndani, asubuhi ya leo, Ndugu na Dada Coats.

14 Sasa, katika Kitabu cha Wakorintho m—mlango wa 10, Kitabu hiki cha Wakorintho ni kitabu cha masahihisho. Tunapaswa kuchukua Kitabu cha Wakorintho. Ndilo kanisa pekee katika Agano Jipya lote, ambalo, inavyoonekana, ambalo viongozi walikuwa na shida sana nalo. Lakini, Wakorintho sikuzote walikuwa katika shida. Paulo, alipokuja miongoni mwao, mmoja alikuwa na lugha, na mmoja alikuwa na zaburi, na mmoja alikuwa na hisia na mhemko. Naye sikuzote alikuwa na shida na hawa Wakorintho, akiwaweka sawa.

15 Tukiangalia, hangeweza kuwafundisha Wakorintho mambo yenye kilindi. Walikuwa tu ni mtindo wa ki—ki—kitoto. Wao—wao... Asingeweza kuwaendea katika jumbe kuu, za kilindi, alizowapa Waefeso na alizowapa Warumi, na kuwafundisha mambo yenye kilindi, kwa maana wasingeweza kuyastahimili. Wa—wao walitegemea sana mihemko midogo na mambo madogo kama hayo. Ati tu, “Vema, Bwana asifiwe, nimeipata! Ni—nilijiwa na u—ufunuo. Nilikuwa na zaburi. Nina unabii.”

16 Naye Paulo akasema, “Mambo haya yote yatashindwa.” Mnaona? Kila moja la hayo, hayapaswi kutumainiwa kupita kiasi. Na kwa hiyo, lakini, anachojaribu kuliletea kanisa, kilikuwa ni hiyo nanga, ambapo sisi—ambapo tuna nanga katika Kristo, ambapo hatutumainii mihemko. Hatutegemei mafunuo. Hatuyatumainii mambo haya. Ila, tunamwamini Kristo. Tunaenda kule kwa imani. Ninii tu. . .

17 Tunaona Paulo angeweza kuwafundisha Waefeso pale, jinsi ambavyo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, walikuwa wamechaguliwa tangu zamani wapate kufanywa wana wenye mamlaka wa Mungu. Sasa, yeye... Wakorintho hawakujua lolote kuhusu hilo. Wao walininii tu... iliwabidi wawe na hisia kidogo, ama chochote kile, mhemuko mdogo, mmoja *huu, ule*, na *mwingineo*. Nao walitegemea hilo. Asingeweza kuwafundisha mambo yenye kilindi.

18 Kwa hivyo, nadhani ni jambo zuri sana unapokuwa na watu ambao unaweza kufundisha mambo yenye kilindi, Naye Roho Mtakatifu anaweza kuzimalizia kweli hizi kuu, na kuziimarisha mi—mionyoni mwa watu, wapate kujua wanaposimama, kuwa na mhemko au bila mhemuko, unabii au bila unabii, na chochote kile, chochote. Ikiwa wao... hatuninii... Sasa kumbukeni, sisi sio... Sijaribu kusema ya kwamba Mungu hashughulikii unabii na mambo kama hayo, lakini hatutegemei hayo. Tuna mshiko wenye kilindi kuliko huo, mnaona. Kwa maana, alisema, “Popote palipo na unabii, utabatilika. Zikiwapo lugha, zitakoma. Na yakiwapo...”

19 Na mihemko hii yote waliyokuwa nayo hao Wakorintho, hakuna hata mmoja wao uliokuwa ni thibitisho la kwamba wameokoka. Hakuna hata mmoja wao ulikuwa ni ushahidi kwamba walikuwa wameokoka. Sivo... Kama ungeweza

kupaza sauti, kama ungeweza kutabiri, kama ungeweza kuwaponya wagonjwa, kama ungeweza kunena kwa lugha, kama ungeweza kufasiri lugha, kama ulikuwa na hekima, na ulikuwa na maarifa, hakuna hata moja kati ya hizo inayomaanisha kuwa umeokoka; si hata moja ya hizo. Unaweza kuwa na kila moja ya hizo, Paulo alisema, katika Wakorintho wa Kwanza 13, na upotee. “Si kitu mimi,” unaona.

²⁰ Lakini, unapokuwa na upendo, nanga! Asubuhi ya leo, kwa yapata muda wa saa moja kabla ya mke wangu kuamka, nilikuwa macho. Naye Bwana alikuwa akinifunulia, jambo fulani kuu kuhusu jinsi Mungu anavyoliunganisha Kanisa Lake pamoja, kwa vifungo hivyo vya upendo, na jinsi linavyopaswa kuwa. Hakuna njia nyingine ya mtu kuokolewa bila kuzaliwa mara ya pili. Mungu akipenda, nataka kuhubiri juu ya hilo juma hili lijalo. Nalo linajitokeza tu wazi moyoni mwangu. Labda Bwana atanipa Ujumbe juu yake.

²¹ Sasa, Ujumbe huu asubuhi ya leo, jinsi ulivyoniija moyoni mwangu mle ndani, ni Ujumbe, onyo. Nami nikawazia, labda, kama tungewaletea watu onyo hili, kama vile Paulo alivyokuwa akiwaonya hawa Wakorintho. Kama tunaweza kuwapelekea watu onyo hili, tukijua ya kwamba tunakabiliwa na uamsho sasa, na wakati wa kuchunguza, wakati hatuna budi kuchunguzwa. Sasa, Paulo alisema:

Zaidi ya hayo, ndugu zangu, sipendi ninyi mkose kufahamu, jinsi ambavyo baba zetu wote walikuwa chini ya wingu, wote wakapita kati ya bahari;

Nao...wote wakabatizwa wawe wa Musa katika wingu na katika bahari;

²² Sasa, anawapa ufahamu ya kwamba wakati Mungu alipowatoa Israeli kutoka nyikani, wakaingia nyikani kumtumikia Yeye, na kuwapeleka kwenye nchi ya ahadi. Wao... Yeye anaweka mfano hapo, kwamba, kama vile tunavyotolewa katika vitu vyote vya kimwili, de—desturi zote, na maagizo, wao walitolewa vivyo hivyo. Nasi tunaona, tukiendelea mbele kidogo katika somo letu, ya kwamba wengi wa hao waliangamizwa. Kwa sababu, wangeweza kufanya desturi zote, na maagizo yote, na kila kitu ambacho Mungu alihitaji, na bado mioyo yao haikuwa sawa na Mungu.

²³ Sasa, tunaweza kufanya mambo mengi. Tunaweza kula ushirika. Tunaweza kubatizwa. Tunaweza—tunaweza kuja kanisani, tuandike majina yetu kwenye kitabu, ama tuwe na heshima na kicho tuwezavyo, na bado tupotee. Hilo ni onyo zito. Tungeweza kuwa tu... kufurahi tu wakati Roho angeshuka, na katika mkutano ambapo Neno lilikuwa likihubiriwa, nazo nafsi zetu zingefurahi tu pamoja na Neno, na bado tumepotea.

²⁴ “Mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki.” Mvua ile ile inayoifanya ngano ikue, huyafanya magugu kukua. Ni asili ya

bidhaa, mnaona. Ni asili yake ndiyo inayotwambia kile tulicho. Kwa hiyo, ni asili iliyo ndani yetu, ambayo hutwambia kile tulicho. Mnaona? Sio. . .

²⁵ Huenda tukawa wa kidini sana hata tusingetumia mikono yetu Jumapili, kufanya jambo lolote. Huenda hata tusishone nguo zetu siku ya Jumapili. Huenda hata tusijisikie kuwa na haki ya kununua chakula Jumapili. Na tunaweza kuwa wa kidini sana na wachamungu sana! Lakini, hata hivyo, ikiwa hatujazaliwa upya kihalisi kwa Roho wa Mungu, tunaabudu tu bure.

²⁶ Kwa hiyo, sasa, ni ngumu sana. Nasi tunataka kweli kulipata na kuijua Kweli. Kwa sababu, kumbukeni, hatutapata nafasi ya pili kwa jambo hili. Ni mara hii moja tu, kwa hivyo afadhali uwe na uhakika kabisa.

Sasa, angalieni, “Sipendi mkose kufahamu, ndugu zangu.”

²⁷ Sasa, Wakorintho hawa, nilisema nini kwanza kabisa? Walikuwa wakiwekea msingi matumaini yao ya Milele juu ya hisia fulani. Paulo alisema, ninii tu. . . Hapo, alisema, “Ninapokuja miongoni mwenu, mmoja ana *hiki*, na mmoja ana *kile*. Na mmoja—mmoja. . .” Kasema, sasa, wote. . . Hilo ni sawa. Hatuna neno dhidi yake. Lakini, bado, hilo silo tunalozungumzia. Mnaona? Hilo silo.

²⁸ Nakumbuka nilipoongoka kwa mara ya kwanza. Nami nikaanza kuona kazi ya Roho, na jinsi ambavyo wengine wangeweza tu kuiga Roho Mtakatifu halisi, wa kweli, na kiasi kwamba, mbona, ilikuwa haiwezekani kabisa kujua ni yupi wa kweli na wa uongo, angalau.

²⁹ Nami nikamwona mtu niliyemjua, nami, na kwa utambuzi, nilijua kuwa mtu huyo alikuwa akiishi na mke wa mtu mwingine. Naye huyu hapa amesimama pale akizungumza kwa lugha na kufasiri, na kila kitu, na kutoa jumbe. Na hiyo. . . Nami nikampeleka huyo jamaa mwingine mahali ambapo ningeweza kuzungumza naye kwa dakika chache, na, ni Mkristo halisi wa kweli.

³⁰ Basi nikawazia, “Huyo Roho anawezaje, Roho yeye yule, ambapo mimi. . .” Hapo ndipo nilipoiona pentekoste kwa mara ya kwanza. Na ilikuwa huko Mishawaka, Indiana. Nami nawaambia, bila shaka. . . Niliwazia, kwa saa chache za kwanza nilizokuwa pale, nilikuwa miongoni mwa Malaika. Kisha saa chache zilizofuata, nilidhania nilikuwa miongoni mwa pepo, nilipoona hilo. Niliwaona watu hawa wawili, mmoja akitoa ujumbe, mmoja akafasiri.

³¹ Sikuwahi kusikia kunena kwa lugha, na mambo kama hayo, hapo awali. Nilizitazama roho hizo, jinsi zilivyotenda kazi. Nikawazia, “Loo, jamani! Mbona, ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu umeanza.” Ndipo nilipopata nafasi, kwa nje, kuzungumza na mmoja wao na ningeweza kujua alivyokuwa hasa, kulikuwa na mmoja mwovu iwezekanavyo.

³² Ndipo—ndipo usiku huo, nikawaangalia tena, nami nikawazia, “Loo, niondoeni hapa. Siwezi kuelewa jinsi hii ilivyo.” Nami nikaona mambo hayo yalikuwa katika Biblia. Lakini huyu hapa mtu aliyekuwa akiyatenda, ambaye hakuwa na Roho wa Mungu; na huyo mwingine akifanya hivyo, naye kweli alikuwa na Roho wa Mungu. Basi nilichanganyikiwa kabisa. Na nikaliacha tu hilo jambo lote lipite.

³³ Ndipo miaka kadhaa baadaye, baada ya yale mafuriko kwisha, nilikuwa ninaenda, nikipanda barabarani kwenda Green’s Mill, Bw. Isler, seneta wa jimbo, huja hapa kanisani, alikutana nami njiani, akanikumbatia, akasema, “Billy, Kristo anamaanisha nini kwako sasa?” Baba yangu alikuwa ametuacha. Ndugu yangu alikuwa ametuacha. Na mke wangu alikuwa ametuacha. Mtoto wangu alikuwa ametuacha. Nami . . .

Kasema, “Anamaanisha nini?”

³⁴ Nikasema, “Bw. Isler, Yeye anamaanisha zaidi ya uhai kwangu.” Nikasema, “Kitu fulani kimetendeka ndani yangu. Miaka michache iliyopita, Kristo alikuja moyoni mwangu. Na mimi—mimi . . . Imekuwa tu zaidi ya mimi mwenyewe. Ni kitu tu ambacho kimetokea. Si kwa sababu nilikuwa mtu wa kidini. Sivyo. Ni jambo tu ambalo Mungu, kupitia neema, alinifanyia.” Nami nikasema, “Ingawa angeniua, ningemtumaini Yeye vivyo hivyo. Na kama nilikuwa kuzimuni, na kulikuwa na kitu kama upendo, kuzimuni, ningali ningempenda.” Ni hayo tu. Ni kitu fulani *hapa* ndani. Yeye ni wa kweli. Nilistahili kila adhabu niliyowahi kupata. Wewe fanya vivyo hivyo. Lakini kama nanga hiyo, hicho Kitu fulani, hiyo nanga ya upendo wa Mungu, inayoshikilia moyoni mwa mwanadamu. Mambo mengine yanafuata.

³⁵ Nikiwa nimeketi kwenye gogo kule juu, nilikuwa nikiomba kuhusu jambo lingine. Ndipo Biblia yangu ikafunguka, nami nilikuwa nikisoma katika . . . kwenye Kitabu cha Waebrania, mlango wa 6. Nami nilikuwa nikisoma hapo, jinsi ambavyo, “Haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, wakianguka, kujifanya upya tena hata wakatubu. Kwa maana mvua huinyeshea nchi mara kwa mara, ili kuinyesha, na kuinyeshea, kwa hao ambao kwa ajili yao yalimwa. Lakini kile kilicho karibu na kukataliwa, miiba na michongoma, iliyo karibu na kukataliwa, itateketezwa.”

³⁶ Naye Roho Mtakatifu akaendelea kusema nami kuhusu hilo. “Hiyo ni nini?” Ningeisoma tena. Ndipo basi ono likaja. Na nikaiona dunia imesimama mbele yangu, ikizunguka. Yote imepigwa haro, na kama kwamba imelimwa na iko tayari kupandwa. Ndipo akapita mtu, mwenye mavazi meupe, akipanda mbegu. Na baada ya kuzunguka mpindo wa dunia, mtu mwingine akaja, mwenye mavazi meusi, akipanda mbegu nyuma yake. Basi wakati mbegu alizopanda mtu mwema, zilipotokea,

zilikuwa ni ngano. Nazo zile mbaya, zile yule mtu mweusi alizopanda, hizo mbegu zikatokea, naye alivikwa mavazi meusi. Zikatokea, nazo zilikuwa ni magugu. Na, loo, moja ilikuwa kinyume na nyingine.

³⁷ Ndipo ukame mkuu ukaja, katika lile ono. Ndipo maskini ile ngano ikainamisha kichwa chake; ilikuwa na kiu sana ya maji. Nalo gu—gugu likainamisha kichwa chake; lilikuwa na kiu ya maji. Ndipo wingu kubwa likatanda, nayo mvua ikanyesha. Ndipo maskini ile ngano ikainuka na kuanza kushangilia, “Bwana asifiwe! Bwana asifiwe!” Ilifurahia sana kupata maji hayo. Kisha maskini lile gugu likainuka, likaanza kushangilia, “Bwana asifiwe! Bwana asifiwe!” kwa ajili ya maji yale yale.

³⁸ Ndipo nikaelewa. Mnaona? Hilo hapo. Roho Mtakatifu atashuka, lakini, “Kwa matunda yao wanatambulikana,” alisema Bwana Yesu. Mnaona? Mnaona? Si kwa matendo ya Roho, kama wanawaponya wagonjwa, ama kama wananena kwa lugha, ama kama wanaimba katika Roho, au kama wanashangilia *hivi* au *vile*. Wanaweza kufanya hayo yote na bado wakapotea. Ni maisha yako ndani yako, lile tukio la kuzaliwa mara ya pili.

³⁹ Sasa, Paulo alikuwa akijaribu kulielezea jambo hili kwa wale Wakorintho. “Mimi . . .”

*Zaidi ya hayo, ndugu zangu, ningependa . . .
nisingependa mkose kufahamu, jinsi ambavyo . . .
baba zetu wote walipitia chini ya wingu, na . . .kupita
kati ya bahari;*

Nao . . . wakabatizwa wawe wa Musa . . .

⁴⁰ Kila mmoja wao alikwenda nyikani. Yesu alisema, “Sio wote wasemao, ‘Bwana, Bwana,’ wataingia. Bali yule afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye Mbinguni.” Sio kile unachosema. Unaweza kuihubiri Injili na bado upotee. Bila shaka.

⁴¹ Haya si mambo ya watoto wadogo tu. Hili kabisa ni . . . Lina kilindi. Nao Ukristo haupaswi kuwa ni kitu kidogo, chepesi tu, cha kujibunia, kama vile, “Vema, nitaenda kanisani, nami najua ni wajibu wangu kwenda.” Huo sio Ukristo. Ndugu, Ukristo sio . . .

⁴² Ni jambo ambalo Mungu amefanya. Mungu amekuchagua wewe, katika Kristo, na kukuwasilisha kama zawadi ya upendo, kwa Kristo. Na kama . . . wito wa Mungu, uteuzi! Na iwapo tuna nafasi ya kuwa mtu wa aina hiyo, na kuukataa, kwa ajili ya maskini mambo madogo madogo ya ulimwengu? Sasa sikilizeni tunapoendelea.

Nao wote wakala mana iyo hiyo ya kiroho;

⁴³ Mlisikia hayo? Kifungu cha 3.

Nao wote wakala mana iyo hiyo ya roho;

44 Anazungumzia nini? Taratibu za kanisa. Watu huja kanisani na kusema wametubu, na kubatizwa katika Kristo, wakilichukua Jina la Bwana Yesu. “Nao walifanya hivyo huko nyikani, pia,” Paulo alisema. Hivyo ndivyo Wakorintho walikuwa wamefanya. Waliingia na kubatizwa katika Kristo. Wakamchukua Kristo, kwa nje. Kitaaluma walikuwa wamemchukua. Kiakili walikuwa wamemkubali.

45 Lakini, ndugu, ni zaidi ya mambo ya kiakili. Linapita hayo. Linaenda kwa—kwa Kuzaliwa halisi, sio tu mawazo ya kiakili au kazi ya mhemuko. Lakini, Kuzaliwa, tukio, kitu fulani kinachoingia moja kwa moja moyoni na kuubadilisha kabisa utu wa ndani, kinachokufanya ufanye mambo ambayo usingefanya, kwa maneno mengine. Kinakufanya uwapende wale ambao hawapendeki. Kinakufanya utende tofauti na vile ulivyowahi kufikiria kwamba ungetenda.

46 Ndipo hali za mambo zinapoinuka, ni nanga yako. Huna haja ya kujiuliza, “Je, nitafanikiwa?” Loo, hapana. Sio kama nitafanikiwa. Tayari imefanywa kwa ajili yangu. Kristo ndani yangu, ameifanya, Mwenyewe, nami ninatumaini tu katika nanga Yake pekee. Ni jambo la ajabu jinsi gani!

47 Angalieni, wote walikula ushirika. Nuru hiyo iliyokuwa ndani. . . Tunajua kwamba ilikuwa ni mchakato wa asili, kwa sababu ilikuwa kitu kama jalidi ndogo iliyonyesha kutoka Mbinguni, mikate midogo myembamba iliyopakwa asali. Ni. . . Huo mkate mwembamba ulikuwa kitu kidogo tu kama biskuti, mkate mdogo, nao ulikuwa umepakwa asali. Na wote walishiriki hiyo. Kila mtu alipitia kwenye Bahari ya Shamu, na kubatizwa katika Wingu na kupitia baharini, wawe wa Musa. Kwa kufuata maagizo yake, kama mtumishi wa Mungu, wote walibatizwa wawe wake. Wote walikuwa wafuasi, kama tulivyo leo hii, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, yule Mwalimu mkuu wa Kanisa la Kikristo. Tunaongozwa kote, kufikia ubatizo wa maji.

Naye akasema, “Wote walikula mana ile ile.” Ninii. . .

48 Ilifanya nini? Mana hiyo ilianguka kwa ajili ya Kora na kwa ajili ya kundi lake, sawasawa tu na vile ilivyoanguka kwa ajili ya Musa, Kalebu, na Yoshua. Wote walikuwa wamechanganyikana pamoja, wote washiriki wa ubatizo, wote washiriki wa ushirika, wote washiriki wa maungamo, na, sasa, wote washiriki wa ushirika.

49 Mnalipata? Angalieni onyo hilo zito. Na, enyi watu wa maskanini, acheni hilo likolee ndani kabisa. Kumbukeni, ni kikomo chako cha Milele, kinaning’inia pale pale. Usilipuuze tu kana kwamba ni maskini mpapatiko mdogo au chochote kile. Hili ni jambo ambalo hatuna budi kulikaribia kwa uchaji. Ni jambo linaloamua kama tutaishi baadaye au la.

50 Wote walibatizwa kuwa wa Musa, kupitia Bahari ya Shamu. Wote walimfuata Mtu yule yule wa Kiroho, lile Wingu na

Nguzo ya Moto. Wote waliongozwa na Malaika yule yule. Wote walitoka na mchungaji yule yule. Wote wakabatizwa baharini. Wote walikula ile mana ya kiroho. Na hiyo mana ilikuwa ni Kristo. Kristo akishuka, hiyo mana ilishuka kila usiku kutoka Mbinguni, na kuangamia hapa, ili kuwadumisha hao watu safarini mwao.

⁵¹ Naye Kristo alishuka kutoka Mbinguni na kuyatoa maisha Yake, ili, “Kila amwaminiye asipotee bali awe na Uzima wa milele.” Kristo alishuka na akawa mana yetu, tupate kula baraka zizi hizi za kiroho.

⁵² Kwa hiyo, Roho Mtakatifu anaweza kushuka moja kwa moja miongoni mwa watu, na Wakristo na walio vuguvugu pia, na waaminio nusunusu na waaminio wakwamia mpakani wote watakula vivyo hivyo. Lakini hiyo haimaanishi hilo bado. Loo, laiti ningalikuwa na maneno, ambayo ningeweza kulishindilia hili ndani na kulikaza moyoni mwa kila mtu hapa. Na kuona jinsi lilivyo jambo lenye kilindi. Sio kitu cha kuchezeza. Sio tu kwenda kanisani.

⁵³ Sasa, sikilizeni. Wote walikula mana ile ile ya kiroho. Wazieni jambo hilo, mana ya kiroho!

⁵⁴ “Loo,” unasema, “najua nimeokoka. Haleluya! Nimepiga kelele katika Roho. Nahisi *hivi*.” Hilo halina uhusiano wowote nalo. Unaona jinsi tunavyowekea msingi kikomo chetu cha Milele juu ya mhemko? Je, unaweza kuona, katika siku hii tunayoishi sasa, jinsi watu wanavyowekea msingi ki—kikomo chao juu ya mhemko mdogo? “Loo,” kasema, “najua ninayo, kwa sababu ni—nilihisi Nguvu zikipitia ndani yangu. Nilifanya *hivi*.” Hiyo inaweza kuwa ukweli mtupu, na ungali bado umepotea.

⁵⁵ Loo, laiti tungalikuwa na muda kidogo. Hebu tufungue tu Wakorintho wa Kwanza 13, hapa, kwa muda kidogo tu, na kusikia yale Paulo anayosema juu yake, papa hapa.

Nijaposema kwa... lugha za wanadamu na... malaika, kama sina upendo (ambao ni kupendana), nimekuwa shaba iliayo, na katika upatu uvumao.

... nijapokuwa na karama ya unabii, na kujua siri zote, na kujua maarifa yote; nijapokuwa na imani timilifu, kiasi cha kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi.

⁵⁶ Msikilize maskini mtume yule mkali akilishindilia katika kanisa hili la kimhemko, ambao wanaweka matumaini yao juu ya mihemko. Sasa, hii ni shule ya Jumapili. Hapa ni mahali pa masahihisho. Hapa ni mahali pa mafundisho. Na ole wake mtu atakayesimama mimbarani na kupotosha. Ndugu, ni wakati ambapo tumelinganisha Maandiko na Maandiko. Hiyo ni kweli.

*Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini. . .
nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo,
hainifai kitu.*

⁵⁷ Tazama, matendo yako yote mema, matendo yako yote mema, mambo yote ya kiroho uliyo nayo, karama zote ulizo nazo, hisia zote ulizo nazo, furaha yote uliyo nayo, amani yote uliyo nayo, haina uhusiano wowote nalo, kwanza kabisa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

⁵⁸ Wazia jambo hilo, kwa muda kidogo tu. Pia yawazie makanisa siku hizi, makanisa yetu makuu, Presbiteri, Methodisti, Baptisti, na ya kimadhehebu, wanafikiri kwa sababu wanasema, “Naamini,” wanaingia, wanaweka jina lao kwenye kitabu, hilo latosha. Jinsi walivyopotea kwa mbali!

⁵⁹ Watu wetu wa Kipentekoste wanafikiri, vema, kwa sababu wana mhemko mdogo, walijisikia vizuri, walinena kwa lugha, walikuwa na damu kidogo mikononi mwao, mafuta kidogo usoni mwao, ama chochote kile, “Tumempata.” Loo, wamepotea umbali wa maili milioni kumi! Mnalipata? Tazama jinsi ibilisi, kama mungu wa ulimwengu huu, ameyapofusha macho ya hao, nao wanaendelea kuishi namna hiyo. Sikilizeni.

*Maana nijapotoa mali zangu zote kuwalisha maskini,
tena nikijitoa mwili wangu. . . niungue moto, kama sina
upendo. . . si kitu mimi.*

⁶⁰ Angalieni karama hizo zote, mambo hayo yote mazuri. “Nawalisha maskini. Ninao moyo mzuri. Mimi hufanya hivi. Mimi hufanya vile. Ninaenda kanisani. Nanena kwa lugha. Ninatabiri. Nawaponya wagonjwa. Ninahubiri Injili. Mimi hufanya mambo haya.” Paulo alisema, “Bado, si kitu mimi.” Mambo hayo yote yanaweza kuigwa kimwili. Sasa anasemaje?

*Upendo huvumilia, . . . hufadhili; upendo hauhusudu;
upendo hautakabari, . . . haujivuni,*

*Haukosi kuwa na adabu, . . . (Wazia tu!) si mwepesi wa
kuona chungu, hauoni mabaya;*

⁶¹ Upendo, kupendana. Upendo ni nini? Ni Mungu. Mungu anakujaje kwako? Kwa Kuzaliwa. Unaona?

⁶² Sasa, wote walibatizwa kuwa wa Musa. Wote walikula ushirika. Wote walikuwa na mana ile ile ya kiroho iliyotoka kwa Mungu. Kila mmoja wao alikula kitu kile kile.

⁶³ Na, leo hii, tunasimama moja kwa moja na kulisikia Neno, na kulifurahia, na kuchukua Mana na kuila, na kusema, “Loo, haleluya! Hilo ni jema. Loo, ninathamini Hilo. Naam, nilibatizwa kanisani. Na—nachukua na kukata kauli yangu. Niliweka jina langu kwenye kitabu. Mimi ni mfuasi mwanzilishi.” Yote hayo ni bure kabisa endapo hakuna kitu ambacho Mungu amefanya. Ikiwa ni. . . Hayo ni mambo uliyofanya wewe. Hayo ni mambo ambayo imani yako ilitoa.

64 Lakini, isipokuwa Mungu amefanya jambo fulani kwako, kwa Kuzaliwa upya! Hebu kidogo sasa. Sasa kifungu cha 4.

Wote wakaunywea Mwamba ule ule wa kiroho: kwa maana waliunywea Mwamba wa roho uliowafuata: na mwamba huo ulikuwa ni Kristo.

65 Wote walikunywa kutoka kwenye chemchemi, wakashangilia. Basi hiyo inamaanisha nini? Ngano na magugu pia yalishangilia kupata maji hayo ya kiroho. Tunaenda kanisani. Tunapiga makofi yetu na hao wengine. [Ndugu Branham anapiga makofi yake—Mh.] Tunapiga makelele pamoja na hao wengine. Tunaruka-ruka sakafuni pamoja na hao wengine. Tunamsifu Mungu pamoja na hao wengine. Tunatabiri pamoja na hao wengine. Tunanena kwa lugha kama hao wengine. Tunawaombea wagonjwa kama hao wengine. Lakini alisema . . . Sasa sikilizeni, tunapoendelea mbele kidogo.

66 Sasa ninii . . . nataka kusimama kwa dakika moja, loo, juu ya, “Mwamba huo ulikuwa ni Kristo.” Huo Mwamba ulikuwa ni Kristo. Ulikuwa pale katika hali halisi, kama ulivyo katika hali ya kiroho leo hii. Ile Mana, Chakula, ambacho ni Neno litokalo kwa Mungu Mbinguni, Kristo ni Neno la Mungu, nasi tunakula Neno. Mnaona? Tunaketi, kama vile katika Ujumbe asubuhi ya leo, tunasikiliza. Nafsi zetu zinalifikia na kulikamata Neno hilo. Tunaishi kwa Neno. Akasema, “Wote walikula Mana ile ile ya kiroho, na wote wakanywa, wote walikunywa kutoka katika Mwamba ule ule wa kiroho, na Mwamba huo ulikuwa ni Kristo.” Wazia hilo.

67 Sasa yeye atafanya nini? Kulimalizia hapa. Anawaonya hao Wakorintho, “Iweni waangalifu yale mfanyayo. Nilipokuja kwenu, mmoja ana zaburi, mmoja ana lugha, mmoja ana *hii*, na mmoja ana *ile*, mmoja ana unabii, mmoja ana ufunuo, mmoja anafanya *hili*, na mwingine anafanya *lile*.” Kuwa mwangalifu. Usiwekee msingi imani yako juu ya hilo. Mambo hayo ni sawa, yana mahali pake, na kanisani, lakini kamwe usiwekee msingi wokovu wako kwenye hilo. Ikiwa maisha yako hayalingani na Neno la Mungu, basi ni wakati wa kujiweka sawa na Mungu.

68 Angalia, sasa, na, Mwamba huu, Mwamba huu ulikuwa ndio ule Mwamba uliokuwa nyikani.

69 Nami nataka muone, wakati Mungu alipomwita Musa, na kumpeleka huko Misri kuwakomboa wana wa Israeli kutoka kwenye nira ya Farao, Yeye alisema, “Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako?”

Naye akasema, “Ni fimbo.”

70 Ndipo akaichukua hiyo fimbo na kuitupa chini, nayo ikawa nyoka. Naye, Musa, akakimbia. Kisha akaiokota, nayo ikawa fimbo mkononi mwake.

⁷¹ Nayo fimbo hiyo, alipofika Misri, aliinyosha juu ya Misri, nao nzi wakatokea. Akainyosha, nayo mapigo yakashuka. Ilikuwa ni hukumu ya Mungu. Hukumu ya Mungu ilikuwa katika kunyooshwa kwa hiyo fimbo.

⁷² Halafu basi, angalieni, kabla fimbo hiyo haijaweza kushikwa. Musa aliweka mkono wake kifua ni mwake, ukawa ukoma.

⁷³ Kama vile kila mtu alivyo, kwanza kabisa, asili yake ni mwenye dhambi. Hakuna njia ya kuliepuka. Umezaliwa katika dhambi, ukaumbika katika uovu, ukaja ulimwenguni ukisema uongo. Huenda uliwekwa wakfu kwenye madhabahu ya kanisa la mama yako. Huenda ulinyunyiziwa. Huenda ulikuwa *hivi, vile*. Lakini wewe ni mwenye dhambi, kwanza kabisa.

⁷⁴ Kisha, kuna mwingine. Mungu alisema, “Rudisha mkono wako kifua ni mwake.” Juu ya moyo wake, akaweka mikono yake tena, kwa agizo la Mungu, ambapo tulizaliwa. Kwanza, mkono wake una ukoma. Ulizaliwa na Mungu, kwanza, mwenye dhambi; si kwa kujichagulia, bali kwa maumbile; kisha unarudi tena. Ndipo alipoutoa, huo mkono ulikuwa safi na mkamilifu, ikionyesha ya kwamba mkono huu, kabla ya kuitikisa fimbo ya hukumu, ilibidi uwe ni mkono uliosafishwa, kabla ya kuweza kutikiswa. Na mhudumu yeyote, mwalimu yeyote . . .

⁷⁵ Nilisikia jambo fulani asubuhi ya leo ambalo kweli lilinishtua, nilipoifungulia redio yangu, kabla tu ya kuja. Hakuna madharau; na kama kuna mtu yeyote hapa, anayehusiana na mtu huyo, sikusudii kukuudhi. Lakini wakati umewadia . . . Na Mungu anisaidie daima kuwa Mkristo vya kutosha kuweka, kufanya kilicho cheusi cheusi, na cheupe cheupe, niwe mwaminifu.

⁷⁶ Nilimsikia mtu fulani akiimba, akasema, “Nina agano langu.” Kisha akafungua na kusoma Maandiko, na kuhubiri kutoka kwenye Zaburi ya kwanza, “Heri mtu yule asiyeketi barazani pa wenye mizaha, asiyekwenda katika njia ya wenye dhambi.” Mnajua alikuwa ni nani? Yule jamaa wa roki, Jimmy Osborne kutoka kwenye redio, akihubiri Injilio.

⁷⁷ Loo, ndugu, kama kuliwahi kuwako na aibu! Mtu kama huyo hana shughuli ya kuingia katika Neno la Mungu aliye hai. Na unamchukua jamaa huyu kwenye Ngoma ya Kihenge cha Bonde la Renfro, yu macho usiku kucha katika shamrashamra za kale, wakipiga makofi na kupiga makelele katika shamrashamra za kale. Kisha kesho yake asubuhi, abadilishe sauti yake na kuongea kama Mkristo. Na, mbona, ni uchafu na kinyaa machoni pa Mungu.

⁷⁸ Mkono unaoitikisa Fimbo hii ya hukumu hauna budi kusafishwa kwa Nguvu na ufufuo wa Kristo. Yeye hana haja yoyote kushughulikia Neno la Mungu. Hata wahubiri wengi wanajaribu kumtetea huyu Elvis Presley, ambaye si kitu duniani

ila Yuda Iskariote mamboleo. Yuda Iskariote alipata vipande thelathini vya fedha; Elvis Presley akapata dola milioni moja na mlolongo wa Makadilaki. Lakini, alisaliti kabisa. Yeye alikuwa mwaminio wa Kipentekoste, kisha akauza haki zake za mzaliwa wa kwanza apate kuwa mwanamuziki wa roki, na amevuviwa na ibilisi. Nami siichezei hata kidogo. Hapana, bwana. Na Yuda Iskariote mamboleo.

⁷⁹ Na, halafu, hata wahudumu wanajaribu kutetea kitu kama hicho. Huku Elvis Presley akisema, “Naam, ninamtumainia Mungu kwa mafanikio yangu yote.” Je, Mungu mtakatifu aliye hai, angewezaje kufanikisha uchafu na ibilisi, kitu kilichopagawa na pepo?

⁸⁰ Hicho kimekuwa kikwazo kikubwa sana ambacho taifa hili hata limeona, ni jamaa kama Elvis Presley ambaye amewapeleka mamilioni ya watu kuzimuni, kwa upuuzi wake mchafu wa kale wa roki. Bila shaka. Siombi radhi yoyote, hata kidogo. Kama unaweza kuniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu, kumbuka, huyo hapo ibilisi aliyefanyika mwili. Kabisa.

⁸¹ Wala Jimmy Osborne na hao wengine hawana shughuli na Neno la Mungu. Wala mtu yeyote anayelitaja jina la Mungu bure, katika shamrashamra na madansi na roki ya kale na upuuzi mchafu kama huo, kuja kwenye mimbara yoyote na kujaribu kulichukua Neno la Mungu.

⁸² Hiyo ndiyo shida na mengi ya makanisa haya siku hizi, utapata baadhi ya maskini hawa wadogo wa bugibugi kutoka sehemu hizi hapa nje. Maskini msichana mdogo ambaye yuko nje akifanya shamrashamra na kufanya roki zote hizi hapa, usiku mmoja; naye anakuja madhabahuni, ndipo kesho yake usiku mnamweka pale juu akiimba wimbo maalum. Baadhi yenu nyie jamaa mnawatoa maskini hao wacheza gitaa huko nje kwenye klabu ya usiku, na kumweka mimbarani, akihubiri, katika majuma mawili.

⁸³ Ndugu, nakwambia, asingehubiri hapa. La, hashu. Hana budi kujifunza, kujithibitisha kuwa mtu wa Mungu, na kujua. Hatuamini katika huku hapa kurukaruka usiku kucha namna hii. Hilo ndilo limeliweka kanisa katika hali liliyomo siku hizi.

⁸⁴ Tunahitaji Ukweli. Neno hili ni Kweli. Hiyo ni kweli. Mkono unaoitikisa Fimbo hii ya hukumu lazima uwe mkono safi. Kabisa.

⁸⁵ Huo mkono wa hukumu wa Musa ulitakaswa, kisha fimbo ikawekwa ndani yake. Nayoy hiyo fimbo ikashuka na kuleta hukumu juu ya Israeli.

⁸⁶ Halafu basi, nyikani, mfano huo mzuri. Nami sina budi kufunga. Mfano huu mzuri, wa wakati kulipokuwa na Mwamba, “nao Mwamba huo ulikuwa ni Kristo.”

⁸⁷ Nao watu waliokuwa wakiangamia walikuwa wakifa, kwa ukosefu wa maji, nao walistahili jambo hilo. Walistahili kufa kwa sababu walikuwa wamenung'unika. Walikuwa wamelalamika. Hawakuwa waaminio, hapo mwanzo. Hawakuwa kitu ila waaminio wa kiakili. Wao. . . Ma—mambo ya kimbinguni yalikuwa yamefanyika, na umati uliochanganyikana ulikuwa umetoka. Hawakuongoka kutoka moyoni mwao.

⁸⁸ Kulikuwa na watatu tu katika hilo kundi, tunaowajua; Musa, Haruni, na Kalebu, na Miriamu.

⁸⁹ Naye Miriamu akaonyesha usaliti wake, pia, alipocheka, kwa sababu Musa alimwoa msichana huyu wa Kinegro. Na akasema, “Kwani hakukuwako na wasichana wengine wa kuolewa, na kadhalika? Angeweza kufanya hivyo.” Basi Mungu hakupendezwa na jambo hilo, ndipo akampiga kwa ukoma.

⁹⁰ Ndipo kaka yake mwenyewe akapiga makelele, akasema, “Je, ungeweza kumwacha dada yako afe katika hali hiyo?”

⁹¹ Ndipo Mungu akamwambia Musa aje mbele Zake. Naye akaenda na kufanya maombezi kwa—kwa ajili ya Miriamu. Hakuishi muda mrefu baada ya hapo.

⁹² Hapana, ndugu. Anachofanya Mungu ni kikamilifu. Hatuna shughuli yoyote, kwa nia zetu, kuweka chochote Kwake. Liache tu jinsi lilivyo. Mungu alifanya hivyo; Mungu alisema Hilo; hilo latosha. Lichukue tu. Sijui ni vipi. . . Kama ningeweza kulielezea, basi ningekuwa sawa na Mungu. Siwezi kulielezea. Ninaliamini tu. Ni hayo tu. Hilo ndilo lote ninaloombwa kufanya. Hakuna mtu anayeombwa kulielezea, kwa sababu ni zaidi ya akili zetu, ni zaidi ya akili zetu. Ni Mungu anayefanya hivyo, kwa hivyo haliwezi kuelezewa. Ninalikubali tu, kwa imani, na kusema, “Ni mali yangu binafsi, na ninaliamini.” Siwezi kulielezea.

⁹³ Jinsi mwamba huu ulivyowekwa pale! Mungu alikuwa na mwamba, ambao ulikuwa umehifadhi maji, mwamba mdogo tu labda haukuwa mkubwa kuliko dawati hilo. Lakini wakati Musa alipoupiga mwamba huu, kulikuwa na maji ya kutosha kutoka kwake kuwanywesha watu milioni mbili. Isitoshe, bali ng'ombe na kondoo wengi na kadhalika kadiri walivyokuwa nao.

⁹⁴ Loo, ninapoona baadhi ya wasanii hawa, wanaochora picha, tone dogo—dogo linaloanguka kutoka mwambani, na mtoto amesimama pale na ndo—ndoo ndogo mkononi mwake! Loo, hayakutokea namna hiyo.

⁹⁵ Yalikuja kwa mifoko mingi inayobubujika. Yaliwanywesha watu zaidi ya milioni mbili, mbali na ngamia zao na wanyama wao wote. “Nao Mwamba huo ulikuwa ni Kristo Yesu.” Mlinganisho mzuri na Yohana 3:16. “Mungu aliupenda sana ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa Milele.”

⁹⁶ Basi angalia kilichotokea. Njia pekee ambayo wangeweza kuyatoa maji hayo kutoka kwenye mwamba huo, ile fimbo ya hukumu ilibidi kuupiga huo mwamba. Ndipo Musa akaupiga huo Mwamba, nayo hukumu ya Mungu ikaupiga huo Mwamba. Na ilipofanya hivyo, ikatoa maji yake.

⁹⁷ Watu walikuwa kabisa... Mungu alikuwa mwenye haki, kwa kuwaacha wafe, kwa sababu hawakumwamini, walikuwa, hawana heshima, walikuwa wavunja amani, hawakustahili kuishi, hata Musa aliwaita “waasi,” kumwasi Mungu, nao walistahili kufa.

⁹⁸ Nasi sote tulistahili kifo kwa sababu tumemwasi Mungu. Mteule... Angalieni, sote tunastahili kufa. Lakini, Mungu ni mwingi sana wa rehema! Kamwe haikumpasa kutufikiria. Lakini, Yeye ni mwenye rehema sana, hata akazichukua dhambi za kila mmoja wetu, na kuzitundika juu ya Mwanawe mpendwa, Kristo; tusije tukaangamia, bali tuwe na Uzima wa Milele. Tungewezaje kuunywea Mwamba huo, halafu tusiwe sawa moyoni mwetu?

⁹⁹ Lakini, ndugu, kuna mamilioni yao, asubuhi ya leo, wanaofanya jambo hilo. Hiyo ni kweli kabisa. Wanatumaini kwa sababu wao ni Wabaptisti, au Wamethodisti, au Wapentekoste. Wanaamini kwa sababu walikuwa na maskini hisia ndogo za kigeni, kwa sababu walinena kwa lugha, kwa sababu walipiga makelele, kwa sababu walicheza, kwa sababu walikuwa na ibada ya uponyaji na Mungu akawaponya wagonjwa, ama jambo fulani wanalolitumainia, kwa sababu walikuwa na ufunuo (ilikuwa ni kweli,) kwa sababu walifanya *hivi*. Mambo hayo ni sawa, hakuna la kusema dhidi yao, lakini hilo halina uhusiano na wokovu wako, si hata jambo moja. Unaweza kumwaga mafuta kutoka kwa mikono yako hadi yafikie galoni, au damu kutoka usoni mwako, na bado isimaanishe chochote. Hiyo ni kweli.

¹⁰⁰ Paulo alisema, “Ningeweza kunena kwa lugha kama wanadamu na Malaika, na bado niwe nimepotea.” Ingawa ningeweza kuwa na hekima na maarifa, na ningeweza kusimama na kuelezea Biblia hiyo, kuifanya tu ionekane, kuifungamanisha tu, hilo bado halina uhusiano wowote nalo.

¹⁰¹ Ndugu, wote waliunywea Mwamba uo huo. “Mwamba huo ulikuwa ni Kristo.”

¹⁰² Hukumu zilikuwa juu ya Kristo, kusudi upate fursa ya kuja na kunywa. Ni wema wa Mungu kwako, kwamba unakuja kunywa. Ni wema wa Mungu kwako, kwamba unakula kutoka kwenye Neno. Wema wa Mungu kwako, kwamba alikuruhusu kubatizwa. Wema wa Mungu kwako, kukufanya raia, kukupa afaa, kukuweka kanisani asubuhi ya leo. Ni wema wa Mungu. Huo wote ni wema wa Mungu.

¹⁰³ Lakini vipi kuhusu wema wako kumwitikia Mungu? Je, uko tayari kusalimisha kila kitu, kila wazo, kila tendo, kila

kitu Kwake? Hivyo ndivyo—hivyo ndivyo Mungu alivyokutendea. Utamfanyia nini?

¹⁰⁴ Angalia, hebu tusome mistari michache zaidi. Basi ni—nitafunga, ili mchungaji aliendee neno lake. Sasa angalieni. “Nao Mwamba ule ule ulikuwa Kristo.” Sasa kifungu cha 5.

Lakini wengi sana katika wao, Mungu hakupendezwa...nao:...

¹⁰⁵ Mnaona? Aliwaruhusu wabatizwe. Aliwaruhusu kula Neno na kuliadini. Aliwaruhusu kupata baraka za kiroho. Aliwaruhusu kunywa kutoka kwenye Mwamba wa kiroho. Yote hayo Mungu alifanya, kwa neema Yake, lakini, hata hivyo, Mungu hakupendezwa nao. Tazama.

...maana waliangamizwa nyikani.

¹⁰⁶ Baada ya matukio haya yote, baada ya ibada zetu zote kuu za uponyaji ambazo tumeona, baada ya miujiza yote mikuu ambayo tumeona ikifanywa, baada ya hisia zote kuu ambazo tumekuwa nazo, za kupiga makelele na kumsifu Mungu, kuunywea Mwamba huo, mahubiri yote mazuri ambayo tumefurahia, na bado tuangamizwe. Yote yamekwisha! “Ondokeni kwangu, ninyi mtenda maovu. Hata sikuwajua ninyi.”

¹⁰⁷ Jichunguzeni! Tuna uamsho unaokuja. Najua hii ni ngumu. Lakini, ndugu, baba yeyote ambaye hatawarekebisha watoto wake si baba mzuri. Hiyo ni kweli. “Kuangamizwa.”

Basi mambo haya yalikuwa mifano kwetu,...

¹⁰⁸ Paulo akizungumza. Je, mnaamini hilo? Ilikuwa ni mfano. Vema.

...kusudi kwamba sisi tusiwe watu wa kutamani mabaya kama wale nao walivyotamani.

¹⁰⁹ Je, ungeweza kuwazia mtu akisimama, ambaye ni mpanda farasi, mcheza santuri, na kucheza nyimbo chafu za roki, kisha, “Kitu fulani kilitokea, nikapata mshtuko mkubwa,” na aina zote hizo za nyimbo chafu za kale ambazo Elvis Presley na watu hawa hucheza, na kisha kurudi na kuiga kuihubiri Injili? Wazienu hilo!

¹¹⁰ Ungeweza kuwazia mwanamume na mwanamke wameketi nje, na huyu mwanamke amelala nje kwenye uga wa nyuma, amevaa maskini nguo chafu, nusu uchi, akijianika mbele za wanaume, na kisha arudi moja kwa moja na kuunywea Mwamba huu wa kiroho, na kupiga kelele na kupiga mayowe?

¹¹¹ Kuna fundisho kuu miongoni mwa watu wa Kipentekoste, la ukombozi wa wanawake. Wamevaa hereni kubwa, ndefu, na—na kuvaa mavazi ya kila aina.

¹¹² Basi jamaa mdogo aliketi mbele ya nyumba yangu, siku chache zilizopita, katika lori dogo, akilia, kwamba mke wake... Mpentekoste, hunena kwa lugha, anatoa unabii. Hakika. Na kusema, “Kanisa zima linavaa kaptura.” Naye... “Anatoka

kwenda mtaani, saa mbili na saa tatu usiku, akiokota vipande vidogo vya sigara ambavyo wengine wametupa, na kuvuta. Na bado anapiga kelele, akimsifu Bwana, na kutoa unabii.”

¹¹³ Nilisimama hivi majuzi kanisani, ambapo mtu mashuhuri wa Mungu, ambaye ninamheshimu sana, naye alikuwa akifichua hili. Baada ya mmoja wa wale watu, ambaye ni mmojawapo wa viongozi wake, akitoka nje, na—naye ana damu hii yote ikimiminika mikononi mwao na kadhalika. Nami nimepwelewa na sauti, kutoka mashariki, kutoka magharibi, nikijaribu kuhukumu kitu hicho, kwa misingi ya Biblia. Wakati, si cha Mungu.

¹¹⁴ Damu yoyote ambayo ingetoka kwa Kristo itakuwa ni Damu ya mwili, basi Mwili Wake uko hapa, basi kule Kuja mara ya pili kumekwisha. Yesu alisema, “Msiamini, wanaposema, ‘Tazama, Yeye yuko nyikani.’ Msiamini, wakati, ‘Yuko hapa.’ Msiamini. Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao wataonyesha ishara na maajabu, hata ingewapoteza walio wateule.” Na nimelikemea kutoka mashariki hadi magharibi.

¹¹⁵ Na hatimaye, kule Pwani ya Magharibi, mzee Dk. Canada, ambaye ni rafiki msiri wangu, alisimama. Na mtu mwingine, ambaye alikuwa meneja wa mtu fulani aliyeanzisha jambo hili, mojawapo ya hatua hizi, akaja huko na kutoa ninii kubwa mno. . . Kasema, “Mafuta safi na damu takatifu. Damu yetu itaonyeshwa leo hii.” Nao walipajaza mahali pale. Naye akaonyesha jinsi, chini ya mshipi wake, alikuwa na sindano mbili zimetokeza chini.

¹¹⁶ Mtu yeyote anajua unaweza kung’oa kidole hiki, wala hakitatoka damu isipokuwa ukikamue au kukibinya. Ukitoboa shimo ndani yake, hakitafanya hivyo, kwa sababu mishipa iko mbali sana na hapo. Basi alipofanya hivyo, alionyesha jinsi alivyofanya.

¹¹⁷ Alikuwa na mafuta *hapa* nyuma, akaweka mikono yake juu yake. Kisha akaja na kusema, “Tazameni mkono wangu, ni kawaida kabisa.” Kisha akasema, “Utukufu kwa Mungu! Haleluya!” Naye akakamua mikono yake namna *hiyo*. Hakika, kulikuwa na damu iliyominywa kutoka kwa vidole vyake. Wakati kila mtu alipokuwa akipaza sauti, alipangusa kichwa chake, na kulikuwa na msalaba. Wakati, mtu mwenyewe aliyekuwa pamoja na yule mtu aliyefanya jambo hilo, hilo hapo, limefichuliwa papo hapo mbele ya wasikilizaji, na pamoja na . . . akaingiza mkono mfukoni mwake, kuonyesha mafuta na kadhalika.

¹¹⁸ Mmoja aliweka moyo ukutani, akasema, “Ukuta huu unapumua Damu ya Yesu. Huo ni moyo wa Yesu.” Maskini Mteksasi mkubwa akaingia ndani, hakuogopa. Kasema, “Kama mtu yeyote angegusa huo, wangekufa.” Walikuwa na kamba.

Wote wana picha zake na kila kitu, huko, ambapo ukuta huu ungetokwa na damu, ukipumua damu kutoka moyoni. Basi jamaa huyu anaingia na kujipenyeza kanisani, yeye na mke wake, wakaosha na kuondoa ile rangi ukutani, na kuketi huko nje na kungoja. Walipokuwa wakiingia mchungaji alisema, “Vema, mnajua, Yesu amekuwa humu ndani na kuuondoa huo.”

¹¹⁹ Akasema, “Yesu hakuwa na uhusiano wowote nalo. Nilifanya hivyo, mimi mwenyewe.” Hiyo ni kweli.

¹²⁰ Imekuwaje? Ni kwa sababu watu si imara, juu ya Neno la Mungu aliye hai. Hivi Biblia haisemi, “Wangeenda kutoka mashariki, kutoka magharibi, kutoka kaskazini, na kusini. Kutakuwa na njaa, si ya mkate na maji pekee, bali ya kusikia Neno la Mungu?” Ni siku ya jinsi gani tunayoishi!

¹²¹ Nasi tunaona sasa ya kwamba makanisa haya yote makuu ya kimadhehebu yanaungana pamoja, na imefikia mahali ambapo huna budi kuwa mfuasi wa muungano huu wa makanisa kabla hata uweze kuwa na redio. Umeondolewa kwenye redio. Jamani, usijali kamwe kuhusu hilo. Na wengine wote wako, pia, na vipindi vyote vya televisheni. Itakubidi kuwa mwanachama wa muungano wa makanisa kabla ya kuweza kufanya hivyo. Na unapofanya hivyo, hufanyi chochote ulimwenguni ila alama ya mnyama, ya Biblia. Haya basi. Unaona jinsi yote yameunganishwa pamoja?

¹²² Loo, Mungu ashukuriwe, kweli kuna Mungu aliye hai. Hakika kuna Bwana wa kweli. Hakika kuna Neno la kweli. Hakika kuna uponyaji wa kweli. Kuna kweli ya mambo haya yote. Lakini, ndugu, kamwe usiweke imani yako juu ya maskini mhemko fulani, juu ya utaratibu wa kanisa, juu ya kula ushirika, juu ya kula kutoka kwenye Mwamba wa kiroho.

¹²³ Unasema, “Najua *hili*, ndugu. Nimemuonja Mungu.” Hiyo inaweza kuwa kweli kabisa. Lakini imeangukia mahali pa namna gani? Hilo ndilo jambo linalofuata. Ilingia kwenye ndoo ya aina gani? “Wenye haki na wasio haki.” Sasa sikilizeni.

Sasa haya . . . yalikuwa mifano, kusudi sisi tusiwe watu wa kutamani mabaya, kama wale nao walivyotamani.

¹²⁴ Tamaa yao ilikuwa nini? Sasa, sikilizeni, ninataka kuendelea tu mbele kidogo, kama mtaniwia radhi.

Wala msive waabudu sanamu, . . .

¹²⁵ Loo, unasema, “Namshukuru Mungu, mimi si mwabudu sanamu.” Ngoja tu kidogo. Hebu tulichunguze kwa Neno. Unasema, “Nisingeabudu sanamu.” Hiyo haimaanishi kwa jumla kuwa unaabudu sanamu. Inakubidi tu kuwa mvivu, pasipo kufanya chochote. Unaenda kanisani, “Naam, hilo ni sawa.” Unarudi nyumbani, hufanyi lolote kuhusu Hilo.

126 Ndugu, mwanamume au mwanamke halisi aliyezaliwa mara ya pili hawezi kusimama kimya. Kuna Kitu fulani ndani yao. Hawana budi kushuhudia. Hawana budi kufanya jambo fulani. Wanalazimika kufanya jambo fulani. Hawawezi kunyamaza. Sikilizeni.

Wala msiwe waabudu sanamu, kama (hao) wengine wao walivyokuwa; kama ilivyoandikwa, Watu waliketi kula na kunywa, kisha wakasimama wacheze.

127 Paulo anazungumzia nini? Mifano. Walibatizwa katika kanisa. Walikuwa na ubatizo sahihi kabisa. Wakati mmoja; mara tatu mbele; kinyumenyume; katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; Yesu pekee; vyovyote ilivyokuwa, walikuwa na ubatizo sahihi, walibatizwa vizuri. Tunazozana na kushikwa na kiherehere, na kubishana kuhusu mambo madogo kama hayo. Ina faida gani? Mnaacha kanuni kuu. Makanisa yetu yamegawanyika, juu ya ubatizo. Hakika.

128 Kisha unasema, “Loo, haleluya! Hawana baraka za kiroho tulizo nazo. Wao ni baridi sana, kawaida. Utukufu kwa Mungu, ninakula Mana halisi ya Mungu. Najua ni Kweli.” Hiyo ni kweli kabisa, lakini hiyo inaleta tofauti gani? Unasema, “Ndugu, mimi. . . Ro—Roho Mtakatifu kweli anashuka kanisani mwetu.” Hilo ni zuri, lakini inaleta tofauti gani kwako, ikiwa wewe si aina sahihi ya chombo anachoshukia? Kumbuka.

129 Loo, unasema, “Mimi ni mwaminifu.” Ndivyo walivyokuwa. Waliacha nyumba zao wakaondoka, hata wakatoa shingo zao nje, kusudi mauti yafuate. Walifanya mengi zaidi ya yale yanayotubidi kufanya. Hilo halikuwahusu hata kidogo. Hebu wazieni.

130 Biblia ilisema, “Wananiabudu bure. Wananiabudu bure.” Ibada ya kweli kabisa, bure. Ilianza wapi? Moja kwa moja kutoka bustani ya Edeni, Kaini. Alimwabudu Mungu sawasawa na alivyofanya Habili, lakini alimwabudu bure. Naam, bwana. “Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu.”

131 Unasema, “Naam, ni kwa nini? Sasa nimetubu. Kwa nini siko sawa? Nilitubu. Nafikiri mimi ni mzuri tu kama mtu mwingine yeyote. Ninaenda kanisani. Nimebatizwa. Napata baraka za Mungu. Ninapenda mahubiri mazuri. Nalipenda Neno la Mungu. Ninapenda kulisoma. Nami ninapata baraka za kiroho, pia. Na, haleluya, ninaweza kutabiri. Ninaweza kunena kwa lugha. Nimefanya mambo yote, ati nawe unataka kusema ‘ni bure?’”

132 Sasa, sisemi ni bure, lakini inawezekana kwamba ingeweza kuwa ni bure. Hiyo ni kweli. Inategemea kile ulicho *mle* ndani, ni kweli, kile ulicho ndicho kinapokea hili. Ikiwa hujazaliwa mara ya pili, ikiwa kwa kweli hakuna kitu ndani yako, basi ni bure. Baraka zote, sina la kufanya. Sasa moja tu zaidi.

Wala tusifanye uasherati, kama wengine wao walivyofanya, wakaanguka siku moja watu ishirini na tatu elfu.

¹³³ “Kufanya uasherati,” yaani uasherati wa kiroho. Kama tungalikuwa na wakati... Shule ya Jumapili imekwisha. Uasherati wa kiroho!

Wala tusimjaribu Kristo, kama wengine wao walivyomjaribu, wakaharibiwa na nyoka.

Wala msinung'unike kama wengine wao... walivyoning'unika, wakaharibiwa na mharibu.

¹³⁴ Kunung'unika, kutamani, kuuchanganya ulimwengu na dini yako, kutoka nje... Mungu anapenda usafi, usafi halisi.

¹³⁵ Asubuhi ya leo, nilikuwa nikizungumza. Nikawazia, “Nini...” Sasa, katika kufunga, niliwazia hili: “Ni nini kitamu zaidi katika maisha ya mwanamume? Ni nini kitamu kuliko kuja nyumbani, wakati amechoka na kudhoofika, akiwa na maskini ndoo yake mkononi mwake, kutokana na kufanya kazi siku nzima, ama kulima, ama chochote awezacho kuwa, kuingia ndani na awe na mke wa kupendeza kumlaki mlangoni? Aketi pajani mwake kwa dakika moja, na kuupangusa uso wake kidogo, na kumbusu shavuni, na kumkumbatia, na kusema, ‘Mpenzi, na—najua umechoka, umefanya kazi kwa bidii sana.’ Anamfariji.”

¹³⁶ Jinsi anavyojua ya kwamba mkono huo, uliomkumbatia, ni wake kabisa. Ni wake. Kamwe haumkumbatii mwanamume mwingine yeyote au tamaa nyingine yoyote. Busu lililo kwenye shavu lake ni kutoka kwenye moyo halisi, safi, mtakatifu ambao unampenda tu, na yeye peke yake. Jinsi inavyokufanya... Najua, inakufanya uweke kifua chako mbele, useme, “Loo, sijachoka sana, hata hivyo.” Unaona? Ndivyo hivyo. Linakufanyia kitu.

¹³⁷ Ninataka kukwambia jambo fulani. Lakini vipi kama busu hilo limewekwa shavuni mwake wala hana imani? Huenda lilikuwa kwenye shavu la mwanamume mwingine. Vipi kama hiyo mikono aliyozungushiwa imekumbatia kila mtu, na bado inatamani kufanya vivyo hivyo? Haitakuwa na maana sana. Hakuna mengi yaliyoshikiliwa hapo. Kwa nini?

¹³⁸ Sasa, hapo mwanzo, walikuwa kitu kimoja. Mungu, alipomuumba mtu, alimfanya mtu wa kuwili, mwanamume na mwanamke pia. Alimtenga, katika mwili; na kumweka hapa duniani, katika mwili, nayo sehemu ya kike ilikuwa ingali katika roho.

¹³⁹ Angalia, rafiki, Mungu alikuwa mwangalifu sana. Loo, jinsi hii... Usiruhusu likuache. Mungu kamwe hakuokota konzi la mavumbi na kumwumba Hawa; angekuwa kiumbe tofauti. Wala yeye si kiumbe. Yeye ni zaotuka. Basi Mungu anaingia ndani ya moyo wa Adamu, ubavu huu, moja kwa moja kutoka chini

ya moyo wake, naye anachukua ubavu na kumfanya mke. Na sehemu yenyewe ya roho ya Adamu ilikuwa ndani ya huyo mwanamke, nao hao wawili ni mmoja; nafsi, mwili, roho, ni kitu kimoja. Wao ni umoja mkamilifu. Mwanamke halisi . . . Na mume halisi, mke halisi, wao ni kitu kimoja, pamoja.

¹⁴⁰ Je, ni mfano wa kitu gani? Kristo, kutoka kifuani Mwake! Si zaotuka, si Mmethodisti, ama Mbaptisti, ama kitu kilichobuniwa na Pentekoste. Hapana, bwana. Lakini kutoka moyoni Mwake Mwenyewe, alimtoa Mpenzi ambaye ni safi na mwaminifu awezavyo kuwa. Yeye ni mwaminifu kama yungiyungi.

¹⁴¹ Angalia, angalia kule nyuma kwa Sulemani akizungumza, “Njoo, mpenzi wangu, tutembea kwenye makomamanga. Upendo wetu na ufurike.” Basi mwaminio halisi anapofungua mikono yake kwa moyo safi, naye anashikilia kwa Kristo, mapenzi hayo ya huyo mpenzi wa Kristo yanaingia kifuani Mwake. Ni Mke Wake, kama vile tu mume anavyomfanyia mke halisi.

¹⁴² Tunapaswa kuwa watu wa aina gani? Je, tunafanya ukahaba, kwa Kristo? Je, tunategemea kitu fulani kidogo, na kuufuata ulimwengu na mambo ya ulimwengu, na wenye nia ya kilimwengu, wala sio ule upendo wa kweli na ibada ambayo tunapaswa kuwa nayo?

¹⁴³ Ungeweza kuwazia, jamani, ungeweza kuwazia mkeo, ndugu, akija na kuketi pajani mwako na virinda vyake vya madaha na gaguro zake na vitu vya lesi, na maskini nywele zake zimetengenezwa, na kupambwa, na kila kitu namna hiyo? Akukumbatie, aseme, “Loo, John, nakupenda tu, *busu, busu, busu*, nakupenda.” Nawe unajua papo hapo kwamba kuna kasoro. Huna imani naye, haijalishi anaonekana mrembo kiasi gani na jinsi amejipamba vizuri. Wewe, kama huna imani hiyo kamilifu naye, kuna kasoro. Hai—hairidhishi shauku hiyo ambayo mwanamume angekuwa nayo kwa mkewe.

¹⁴⁴ Na sasa hebu jiwazie tu wewe mwenyewe ukijipumbaza na ulimwengu na kufungamana na ulimwengu, na kupiga magoti yako, useme, “Ee Bwana Yesu, nakupenda.” Ni busu la kinafiki la Yuda, linalowasha. Hiyo ni kweli. Wazieni mambo haya. Kuna uamsho ujao sasa. Mnaona?

¹⁴⁵ Loo, unaweza kuwa umevaa pete ya arusi, hiyo ni kweli, lakini wewe si mke. Loo, unaweza kuwa mwanamke. Unaweza kuwa ndiye mama wa nyumba, lakini wewe si mke ukitenda hivyo.

¹⁴⁶ Nawe si Mkristo halisi, wewe si bidhaa halisi ya Kristo, kama humpendi katika kila kitu ulicho nacho ndani yako.

¹⁴⁷ Sijali kama unaonekana mrembo, kama hu mrembo, unampenda na unajieleza. Hapo ndipo nyinyi wawili mnakuwa kitu kimoja; hapo ndipo Kristo na Kanisa Lake. Si kwa madhehebu, si kwa ubatizo, si kwa mihemko; si kwa chochote ila

kwa upendo wa kweli ulinunuliwa, kutoka kifuani mwa Mungu, alipojeruhiwa pale na akakununua. Na upendo wako, na ukweli wako, na uaminifu wako, unathibitisha jinsi ulivyo. Unaona ninachomaanisha? Iwe umejaa madoadoa ya ngozi kutokana na jua, au uwe. . .

¹⁴⁸ Sijali kama mke wangu kamwe hatachanua nywele zake, kama hakuvaa vazi zuri, au kamwe. . . Hapo, angekuwa mpenzi wangu. Ninampenda kwa sababu ya uaminifu wake, wema wake. Kile alichu, hivyo ndivyo alivyo.

¹⁴⁹ Na kwa Wakristo wanaume na wanawake, hivyo ndivyo tulivyo machoni pa Mungu. Sio kwa sababu tunaweza kwenda kwenye kanisa bora zaidi, au tunaweza kuvaa vizuri zaidi, au tunaweza kuingia katika ujirani *huu*, ama tunaweza kufanya *hili*, ama tunaweza kuendesha *hili*, ama tunaweza kufanya *hili*, *lile*. Hilo halina uhusiano wowote nalo. Ni sifa ya uaminifu wetu na upendo wetu kwa Kristo. Na huko ndiko Kuzaliwa. Hicho ndicho kitu kinachokuja.

¹⁵⁰ “Na nijaponena kwa lugha za wanadamu na Malaika; si kitu mimi. Nijapowalisha maskini; nijapotoa mali yangu; nijapofanya *hivi*, na kufanya *vile*, na kufanya *vile*; si kitu mimi.” Kristo anajali nini kuhusu yote unayoweza kufanya, na yote unayoweza kufanya namna hiyo, ikiwa upendo huo halisi wa kweli na uaminifu haupo? Wazia hilo, sivyo?

¹⁵¹ Hii ni shule ya Jumapili, na, kumbukeni, hilo ni somo kwenu. Kuwa, moyoni mwako, acha Kristo apate nafasi ya kwanza, kama vile mwanamke halisi angefanya kwa mumewe. Hakuna mikono mingine ingeweza kungusa, popote. Hakuna busu lingine, haidhuru linaonekana la kupendeza jinsi gani, naye angegeuza kichwa chake. Ana seti moja ya mapenzi, na hiyo ni kwa ajili ya mumewe. Hiyo ni kweli. Haidhuru mwanamume anaweza kuwa ni mwenye sura nzuri jinsi gani, na jinsi nywele zake zinavyong’aa na ni laini, na jinsi anavyoweza kujishikilia vema. Hapana, bwana. Si hata jambo moja. Anampenda mume huyo, na huyo ndiye pekee anayempenda. Anaacha sifa zake zote na busu zake zote, mapenzi yake yote na kila kitu ni kwa mumewe, naye pekee. Mnaona ninachomaanisha?

¹⁵² Nawe unaacha kila kitu cha ulimwengu, haidhuru kinaonekana ni kizuri jinsi gani, kinaonekana cha kupendeza jinsi gani, na jinsi kinavyoonekana cha kuvutia. Maadili yako ndiyo unayohesabiwa.

¹⁵³ Kisha unasema, “Loo, haleluya! Na—najua niliipata, kwa sababu nilifanya *hivi*. Haleluya!” Huku una hasira ya kutosha kupigana na msumeni.

Hebu nikwambie, ndugu, inahitaji maadili ambayo Kristo anaheshimu.

¹⁵⁴ “Nijaponena kwa lugha za wanadamu na Malaika; nijapomwaga damu kutoka kwa mikono yote miwili; nijapopiga

makelele na kucheza, katika Roho; nijapolila Neno la Mungu, na kulipenda; nijapounywea Mwamba ule ule wa kiroho ambao wengine wao wanaunywea; nijapopiga makofi, kwa sauti kubwa kama wengine.” [Ndugu Branham alipiga makofi—Mh.] “Ingawa naweza kulia machozi ya uongo; ingawa naweza kufanya *haya* yote! Lakini kama hiyo fadhila halisi, ya kweli, halisi ya Kikristo haipo kwa Kristo, unakuwa kama shaba iliayo na upatu uvumao.” Paulo alikuwa akilionya kanisa lake juu ya hili, kanisa la Korintho, ambalo, lilikuwa limechanganyikana kabisa katika kila namna ya mambo ya ulokole.

¹⁵⁵ Ninawaonya, enyi marafiki. Kumbukeni, itanibidi kuwawajibikia kule kwenye Siku ya Hukumu, wala damu yenu haitakuwa juu yangu. Haijalishi jinsi ulivyo mwaminifu kwa kitu kingine chochote, kuwa mwaminifu kwa Kristo. Kumbuka hilo, tunapoomba.

¹⁵⁶ Baba mbarikiwa wa Mbinguni, katika hali hii ya sasa, tunakuja sasa na kukiri makosa yetu yote. Loo, Ewe Mungu mwenye rehema, mwenye rehema. Nasi tunaomba ya kwamba utaangalia chini ndani ya mioyo yetu. Na katika saa hii tunapongojea, huku vichwa vyetu vimeinamishwa kuelekea mavumbini, angalia ndani ya moyo wa mzee, ndani ya moyo wa wanawake wakongwe, ndani ya mioyo ya watu wa makamo, na vijana, hata watoto wadogo. Na tujichunguze.

¹⁵⁷ Tunaingia katika juma hilo takatifu ambalo tunaadhimisha kama Ijumaa Kuu na Pasaka, ufufuo. Ingawa mwaka huu tungeweza kuwa waaminifu kwa kanisa, ingawa huenda tulikula ushirika, ingawa huenda tulipaza sauti, huenda tulifanya mambo mengi, lakini, Ee Mungu, angalia chini ndani ya moyo wangu. Ninazungumza kwa niaba yangu mwenyewe. Angalia ndani ya moyo wangu na ndani ya moyo wa watu hawa hapa asubuhi ya leo, na utuchunguze, Bwana. Kama kuna kitu kinachochukua mahali pa Kristo, Ee Mungu, kiondoe. Ikiwa ni uvivu, kutotosheleza tu, ikiwa ni chochote kinachoweza kuwa, sijui. Lakini, Mungu, kiondoe kwetu. Loo, hatutaki kuangamizwa papa hapa wakati wa vita, kuangamizwa na Mungu na kuwa adui Kwake.

¹⁵⁸ Ee Mungu, angalia ndani ya mioyo yetu. Utuchunguze kwa Roho Wako Mtakatifu, na hebu tuone, asubuhi ya leo, iwapo kuna jambo lolote ovu ndani yetu. Kama lipo, liondoe, Baba. Sasa tunaliweka juu ya madhabahu, ili tuondoke na kuliacha pale. Ikiwa ni uvivu, ikiwa ni hasira, ikiwa ni kutojali, ikiwa ni kupuuza, ikiwa ni chochote kile, ikiwa ni chuki, ikiwa ni kijicho, ikiwa ni ugomvi, kama ni chochote kile, Ee Mungu, kiondolee kwetu, leo hii.

¹⁵⁹ Na kwenye uamsho huu ujao, jalia tujazwe sana na haiba Yako, Bwana, mpaka wengi wataingia na kuokolewa, jumuiya hii ndogo hapa, ambapo tulijaribu sana. Uamsho wa kwanza

sasa katika miaka kumi, ambao nimeufanya. Sasa, ninaomba ya kwamba utatupatia hiyo roho halisi, halisi mioyoni mwetu.

¹⁶⁰ Na itie nanga hapo kwa ajili ya Umilele. Tujalie, Bwana. Utufanye tujichunguze, sisi tuliofunga ndoa, jinsi tunavyowatendea wake zetu, jinsi tulivyo wakweli, au jinsi wake zetu walivyo wakweli kwetu. Na jalia lingie mioyoni mwetu, asubuhi ya leo, jinsi tungewazia kama jambo kama hilo lingetukia nyumbani mwetu. Na kisha jalia tuelekeze mapenzi yetu Kwako, na tuseme: “Ee Mungu, unirehemu.”

¹⁶¹ Loo, kama—kama mkeo angekuja, takribani mara moja tu kwa mwezi, kuja tu na kuweka mkono wake juu ya wako, na kusema, “Mpenzi, nakupenda,” na kuendelea mbele, loo, jinsi ingeonekana alikuwa akinipuza, jinsi ingeonekana kuwa kuna kasoro. Na Mungu, wakati labda mara moja kwa mwezi, au mara moja tunapoenda kanisani, tunaomba maombi kidogo! Loo, Wewe unataka upendo wetu, ushirika we—we—wetu, wakati wote, na mawazo yetu na nia zetu za moyo wetu zitakaa Kwako. Tujalie, Bwana.

¹⁶² Loo, idumishe mioyo yetu imeelekezwa Kwako sana, hata mambo ya ulimwengu yatakuwa vipofu na ya kutojali sana. Tujalie, Bwana. Tusikie sasa, na utubariki katika sehemu inayofuata ya ibada hizi. Tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

¹⁶³ Sasa, Bwana awabariki, vizuri sana. Nami... Samahani nilichukua dakika chache za ziada baada ya shule ya Jumapili kumalizika. Nami naomba kwamba Mungu atawabariki. Sikusema mambo haya; hii ni nje ya Neno la Mungu. Walikuwa mifano kwetu. Wao ni mifano.

¹⁶⁴ Na sasa, angalia, rafiki, ungejisikiaje kama ungejua mke aliyekuwa akikubusu alikuwa ni msaliti? Wazia hilo. Lichunguze hilo kwa muda kidogo. Je, ungewaziaje?

¹⁶⁵ Sasa unapomjia Mungu, na u msaliti, usifanye hivyo. Tuwe wa kweli. Haikubidi kuchukua mhemko. Haikubidi kuchukua kitu tofauti, wakati anga nzima imejaa upendo wa kweli wa Mungu. Kwa nini kuchukua mbadala wakati tunaweza kupata kilicho halisi? Ni kwa ajili yako. Sasa Bwana na akubariki, ninapoirudisha ibada kwa mchungaji wetu.

¹⁶⁶ Na msisahau juma hili, sasa, uamsho huo mdogo ni wa jumuiya na miji midogo iliyo hapa karibu. Nenda kwenye simu yako, mpigie mtu fulani, mwambie atoke nje. Tutakuwa na miito ya madhabahuni, na kutarajia wakati mzuri, juma hili, katika Bwana.

¹⁶⁷ Bwana awabariki mpaka nitakapowaona Jumatano hii ijayo usiku. 🐦

57-0414 Wakorintho, Kitabu Cha Masahihisho
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org